inayochangiwa na neno ‘English’ yaani Kiingereza. (Gachinu na Gachui 1984).

Kuna sababu kadhaa zilizochangia uchipukaji wa Sheng’ miongoni mwa vijana. Sababu kuu ilikuwa kukidhi haja ya mawasiliano baina ya vijana. Changamoto za kiuchumi katika sehemu za mitaa ya mabanda jijini Nairobi zilibidi wapangaji waishi kwenye vyumba vidogo kama makazi yao. Watoto na wazazi walitangamana na kuishi pamoja, katika mazingira finyu. Hali hii ilikuwa ngumu kwa vijana na ilitinga uhuru wao wa mawasiliano yaliyohitaji faragha. Ilibidi wabuni msimbo utakaowawezesha kuzungumzia masuala yaliyowahusu kuambatana na tamaduni za kijamii (Mbaabu na Nzunga 2003).

Sababu nyingine ni ya kisaikolojia ambapo vijana waliweza kujitambulisha kama kundi maalum linalokuwa na mitazamo tofauti na makundi mengine. Falsafa yao ya maisha ilidhihirika kupitia muziki wa kizazi kipya, mavazi mbalimbali pamoja na matumizi ya Sheng’. Sheng’ iliweza kuleta umoja baina yao kama vijana na kuvunja mipaka ya kikabila, kiuchumi na hata kidini. Kundi hili lilipitia changamoto nyingi kama vile kukosa ajira, kukosa mali na hata madaraka serikalini na katika jamii kwa jumla. Hali hii ilibainishwa bayana kupitia matumizi ya Sheng’, msimbo waliouona kama rasilmali yao wenyewe. Hoja hii inatiliwa uzito na Mokaya (2005) ambapo anasema kuwa vijana wengi wa mijini wanatumia Sheng’ kama lugha yao ya kwanza.

Ubunifu wa wanasheng’ umeendelea kukua kila uchao. Kuna msamiati unaozidi kuongezeka siku baada ya siku huku wasemaji wake wakizidi kupanuka kila wakati. Ubunifu wao umeimarika zaidi katika utohozi wa maana. Kuna viwango kadha vya utohozi maana kama vile upanuzi maana, tafsida, ufinyizi maana na usogezi maana. Mbinu hizi zinachunguzwa kwa kina katika sehemu inayofuatia.

## TARATIBU ZA UTOHOZI MAANA

Mwihaki (2006) anafafanua utohozi wa kileksia kama njia ya kuelezea mabadiliko ya kisemantiki ambapo maana awali hubadilishwa kwa njia fulani bila kugeuza umbo la neno. Hivi ni kusema kwamba neno la kukopwa linafasiriwa upya ili kurejelea maana yenye ulinganifu wa kimatumizi na maana ya awali. Umbo la neno huweza kubadilika wakati mwingine, ingawa msisitizo unawekwa kwenye mabadiliko ya maana. Utohozi wa aina hii hufanyika katika maneno ya Sheng’ hasa yale yanayotoholewa kutoka lugha changizi. Wanasheng’ huwa na taratibu kadhaa za utohozi wa maana katika lugha. Sehemu hii itachanganua taratibu tatu zinazohusika katika utohozi huu mathalan:

1.0. Usogezi maana
2.0. Upanuzi maana
3.0. Ufinyizi maana

### 1.0 Usogezi maana

Usogezi maana ni mojawapo wa mbinu za utohozi ambapo maana leksia husogezwa kwa neno katika lugha pokezi (Lehmann 1962). Maana ya dhana za Sheng’ hufafanuliwa kwa kutumia maneno ya lugha changizi ambayo huwa na tofauti za kileksia. Mfano neno la teke katika Kiswahili sanifu hutumiwa kurejelea pigo la mguu. Neno hili hutumika sana kwa mfano katika msemo; ahsante ya punda ni mateke’. Hata hivyo katika Sheng’, teke hurejelea mwanamke, hasa aliye mrembo. Wanaume wengi nchini Kenya hutazama urembo wa mwanamke kupitia umbo la miguu, isiwe miembamba au mipana zaidi. Tunatambua kwamba maana ya *teke* imesogezwa kuelezea dhana tofauti katika muktadha huu.

Ubunifu wa aina hii haujajifunga tu katika sehemu moja ya leksia bali hutumika katika nyanja mbalimbali za mawasiliano. Pesa hurejelewa kama *doo* au *manyamoo*. *Doo* ni neno la Sheng’ lililotokana na neno la Kiingereza *dough* ambalo humaanisha unga uliochanganywa na maji tayari kwa kuokea mkate. Wanasheng’ hulitumia neno hili kumaanisha pesa. Uwezekano wa kununua unga utakaotumiwa kutengenezea mkate unahitaji mnunuzi awe na pesa za kutekeleza jambo hili. Mantiki ni kuwa mtu anapokuwa na pesa ni sawa na kuwa na chakula chenyewe kinachowakilishwa na unga huu. *Manyamoo* kwa upande mwingine ni neno lililotokana na lugha ya Gikuyu linalotumiwa kumaanisha vitu vingi. Wanasheng’ hulitumia kumaanisha pesa kwa sababu mtu anapokuwa na pesa huweza kuwa na uwezo wa kununua vitu vingi. Kuna njia mbalimbali zinazofafanua usogezi maana katika lugha. Baadhi ya njia hizi ni pamoja na:

1.1. Istiari
1. 2. Metonimu
1. 3. Sinedochi

### 1.1 Istiari

Istiari hurejelea matumizi ya neno ambapo maana yake hutumiwa kurejelea maana nyingine. Antilla (1972) anafafanua istiari kama uhusiano wa kimaana kwa mujibu wa matumizi yake baina ya dhana mbili. Mbinu hii ni muhimu katika sarufi za lugha kwa kuelezea dhana mbalimbali. Katika muktadha huu, istiari hutumika kurejelea ule uhusiano wa kisemantiki baina ya Sheng’ na lugha changizi ambao ni wa kiishara, yaani si wa moja kwa moja, Mfano:

| (1.1) Data | lugha changizi | tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *garaji* | Kiingereza | gereji |
| *manzi* | Kiswahili | nyumba |
| *kenge* | Kiswahili | mjusi |
| *kuro* | Gikuyu | mbwa |

Neno *garaji* la Sheng' limetoholewa kutokana na neno la Kiingereza *garage* linalomaanisha ile sehemu ya kuegeshea magari. Linatumiwa kurejelea ile sehemu ambayo magari hutengenezewa yanapoharibika. Wanasheng' hata hivyo wanatumia dhana hii kurejelea hospitali ya kujifungulia kwa akina mama. Mwanamke anapokuwa na mimba huwa ameharibika kiumbo na haonekani akiwa mrembo. Anapofikia wakati wa kujifungua, hulinganishwa na ule utaratibu wa kurekebisha magari kwa kurudishiwa hali yake ya urembo tena.

*Manzi* ni neno la Sheng' lililotokana na Kiswahili. Neno hili limetoholewa kutoka kwa neno manzili katika lugha ya Kiswahili. Linatumika kumaanisha maskani, nyumba au makazi ya mtu (Mohammed na Mohammed 2002). Wanasheng' wanalitumia kurejelea marafiki zao wa kike au wasichana warembo. Wanamhusisha msichana mzuri na ile hali ya mapumziko, furaha na raha wanayokuwa nayo wakiwa nyumbani kwao. Wanamuona msichana mzuri kama ishara ya ukamilifu wa nyumba yao kwani wawili hawa wanatosha kuanza familia.

Neno lingine lililotumiwa kumrejelea msichana mzuri ni *kenge*. Neno hili limetoholewa kutokana na lugha ya Kiswahili ambapo linarejelea aina ya mjusi mkubwa. Mnyama huyu kwa kawaida huwa nadra kumpata kwa sababu huwa akijificha ili asionekane. Wanasheng' wanatumia dhana hii kuonyesha jinsi ilivyo vigumu kumpata msichana mzuri anayewafaa. Kwao kumpata mpenzi si kitu rahisi.

Neno *kuro* limetokana na lugha ya Gikuyu. *Kuro* katika lugha hii hutumiwa kurejelea mnyama anayeitwa mbwa kwa Kiswahili. Mnyama huyu kwa kawaida huwa anafugwa nyumbani na huwa na tabia ya ulafi na hakubaliwi kuingia nyumbani hasa katika tamaduni nyingi za Wakenya. Ni mnyama mwenye tamaa nyingi ya chakula na ngono. Hii ndio sababu mbwa jike hujamiiana na majibwa tofauti kila mara. Wao hawana ubaguzi wa mahusiano ya kimapenzi. Tabia hii ya mbwa ndiyo inayotumiwa kumuelezea mwanamke mwenye tabia ya umalaya anayeonekana kukosa maadili na uwajibikaji wa kimapenzi.

**1.2 Metonimu**

Metonimu ni dhana inayotumiwa kuelezea mabadiliko ya maana ya neno ili ihusishe maana zingine ambazo hazikuwepo awali. Dhana pana ya lugha hutumiwa kuwakilisha ile dhana dogo (Bynon 1977). Metonimu ni dhana pana inayohusisha maana zaidi ya moja, mfano:

| (1.2) | Data | lugha changizi | tafsiri |
|---|---|---|---|
| | *mundu* | Gikuyu | msichana |
| | *mlami* | Kiswahili | mzungu |
| | *gava* | Kiingereza | Polisi |

Katika lugha ya Gikuyu neno *mundu* hutumika kumrejelea binadamu yeyote yule awe mtoto, mzee, mke au mme. Wanasheng' wanapolitumia neno hili hurejelea msichana mrembo hasa mpenzi wao. Msukumo wao katika matumizi haya ni kuficha ukweli kwa hadhira pana. Wasiokuwa na ujuzi wa Sheng' wanaweza kupumbazwa na mada za wanasheng' kuendelezwa bila yao kung'amua kinachorejelewa.

Wazungu wanahusishwa na ustaarabu pamoja na maendeleo ya kiuchumi. Wanasheng' wanaamini barabara za wazungu hawa ni za lami na zisizokuwa na mashimo wala vumbi. Neno *mlami* hivyo basi hutumika kurejelea mzungu kwa sababu anahusishwa na hali hii, tofauti na maana yake ya awali ambayo ni ya kijumla zaidi.

Kenya kama zilivyo nchi nyingine huwa na serikali inayotawala. Nguvu za serikali hii huwakilishwa na maafisa wa usalama kwa njia ya wazi zaidi kuliko idara zingine. Wanaruhusiwa kutumia nguvu, kushika watu, kuwashtaki na hata kuua wakati mwingine. Mara nyingi huwa na magari yaliyo na nambari za serikali pamoja na sare zao zenye nembo ya serikali tawala. Neno la Sheng' *gava* lilitoholewa kutokana na neno la Kiingereza *government* kurejelea mfumo mzima wa kiserikali. Katika muktadha huu hata hivyo, linatumiwa kurejelea polisi wala sio mfumo wote wa kiserikali kama ilivyofafanuliwa.

**1.3 Sinedochi**

Sinedochi huchukuliwa kama mojawapo wa sehemu ya metonimu. Hata hivyo inatofautiana na metonimu kwa kuwa, sehemu ndogo ya dhana hutumiwa kuwakilisha ile sehemu nzima. Dhana yenye maana finyu hutumika kuwakilisha maana pana, Mfano:

| (1.3) Data | lugha changizi | tafsiri |
|---|---|---|
| *karao* | Kiswahili | polisi |
| *keroro* | Gikuyu | pombe |
| *guoko* | Gikuyu | vita |

*Karao* hapa limetoholewa kutoka kwa neno la Kiswahili *karai*. Katika Kiswahili *karai* ni chombo cha chuma kinachotumiwa kukaangia vitu au kufulia nguo. Polisi wa kuzima ghasia hutumia chombo cha aina hii kujikinga wakati wa ghasia. Wanasheng' wanaamisha maana ya chombo hiki kurejelea polisi. Utohozi wa kifonolojia hutokea na kubadilisha jina hili kutoka *karai* hadi *karao*.

Lugha ya Gikuyu hutumia neno *keroro* kurejelea kitu kichungu katika mfano wa pili. Wanasheng' wamelitohoa kutoka maana yake ya kitu kichungu kurejelea aina yoyote ya pombe. *Keroro* pia hutumiwa kuonyesha ile hali ya kulewa. Kwa mfano mtu anaposema: *niko keroro* humaanisha kuwa amelewa chakari.

*Guoko* ni neno lililotoholewa kutoka kwa lugha ya Gikuyu ambalo hutumiwa kurejelea sehemu ya mwili au kiungo kinachotokeza kwenye bega na ambacho hutumiwa kushikia vitu. Kiungo hiki hutumiwa pia wakati watu wanapopigana. Wanasheng' hulitumia neno hili kurejelea hali ya vita, kwa sababu watu hutumia ngumi kupigana au kujikinga.

Hoja zilizojadiliwa zinadhihirisha mbinu ya usogezi wa maana katika Sheng'. Hali hizi zinadhihirisha ubunifu wa lugha. Suala muhimu ni wakati ambapo msamiati mpya unakopwa kutoka lugha changizi na kupata kitambulisho chake katika lugha pokezi kupitia usogezi maana. Dhana mpya katika msimbo wa Sheng' huweza kupata ufafanuzi wa haraka na wenye mantiki kupitia mbinu hii. Mbinu nyingine ni ya upanuzi wa maana kama inavyodhihirika katika sehemu inayofuata.

## 2.0 Upanuzi maana

Lyle (1998) anafafanua upanuzi wa maana kama mbinu ya kuongeza maana kwa nomino ili zitumike katika miktadha mipana zaidi ya awali. Mbinu hii hutumika zaidi katika lugha zote za ulimwengu. Mifano ifuatayo inabainisha matumizi ya mbinu hii katika lugha ya Sheng'

**(1.4)**

| Data | lugha changizi | maana katika Sheng' |
|---|---|---|
| *chuo* | Kiswahili | shule yoyote ile |
| *kizee* | Kiswahili | msichana, mvulana au mzazi |
| *manyake* | Kiswahili | mrembo, nyama, uchi wa kike |
| *punju* | Sheng' | busu, mwizi, mjinga |

Maneno yaliyotolewa hapo juu hupatikana katika miktadha mbalimbali ya usemaji baina ya wanasheng'. Neno *chuo* limetokana na neno la Kiswahili linalomaanisha shule kubwa kuliko sekondari, kama vile chuo cha walimu, chuo kikuu au chuo cha matibabu. Wanasheng' hata hivyo wanatumia neno hili kurejelea mahali popote pa masomo pawe chekechea, shule ya msingi, sekondari au hata shule kubwa kuliko sekondari. Maana ya neno hili yamepanuka kuhusisha shule hizi zote katika matumizi. Hili linatokana na mantiki kwamba shule hizi zote hutoa masomo kwa wanafunzi mbalimbali. Hali hii ya kuwa wanachuo wote huwaunganisha kama kundi maalum.

*Kizee* ni neno lililotokana na neno la Kiswahili mzee lenye maana ya mtu aliyeishi miaka mingi aghalabu kupita hamsini. Mtu huyu anaweza kuwa akiheshimika kwa ajili ya cheo chake. Neno hili linapotoholewa katika Sheng', linawekwa katika ngeli ya 7/8 inayowakilisha vitu visivyo hai. Ngeli hii pia huonyesha udogo wa dhana katika lugha ya Kiswahili. Mfano mtoto mdogo ataitwa kitoto, mtu mdogo ataitwa kijitu. Neno *kizee* linapotumika katika Sheng', huwa na maana tofauti kulingana na muktadha. Maana ya kwanza ni pale linapotumiwa kumrejelea mtu mzima aliyewaudhi. Linapotumika katika hali hii, huwa linaonyesha chuki kwa sababu ya kuwavuruga au kuwaharibia starehe zao. Maana ya pili ni pale linapotumiwa baina ya vijana wa kiume. Muktadha huu wa pili unaonyesha heshima na kuelewana. Neno hili vilevile huweza kutumiwa kumrejelea mpenzi wa kike wa mvulana ambapo linatumika kuficha ukweli kwa waliozoea maana za hapo awali. Upanuzi wa maana unatokana na ufafanuzi wa maana mbalimbali zinazohusu mapenzi, uhusiano wa watoto na wazazi wao pamoja na uhusiano wa vijana wao kwa wao.

Neno *manyake* limetokana na lugha ya Kiswahili. Lilitoholewa kutoka kwa neno nyama katika Kiswahili sanifu. Neon hili huwa ni sehemu laini ya mnyama ambayo hutoa damu inapokatwa na hupikwa ili kuliwa kama kitoweo au chakula maalum. Neno hili hata hivyo linapotumika katika Sheng' humrejelea msichana mrembo. Anafananishwa na nyama au kitu kitamu. Pili neno hili hutumiwa kurejelea sehemu zake za mwili zilizonenepa. Maana ya tatu inatumiwa

kurejelea uke. Hapa maana ya neno hili imepanuliwa kufafanua hali mbalimbali katika usemaji.

Upanuzi mwingine wa maana unaonekana pale ambapo maneno ya viumbe vilivyo hai vinatumiwa kufafanua dhana ambazo hazina uhai au hali mbalimbali za watu, vitu au mazingira. Mfano:

**(1.5)**

| **Data** | **kategoria ya dhana** | **maana** |
|---|---|---|
| *Jordan* | binadamu | kunyolewa kabisa |
| *Muruthi* | mnyama | gari |
| *Rambo* | binadamu | mtu yeyote mkali |
| *Njogu* | mnyama | shilingi elfu moja |

Mfano wa kwanza unatokana na jina la mmarekani anayeitwa Michael Jordan. Mtu huyu alikuwa mashuhuri sana katika uchezaji wa mpira wa vikapu. Huu ni mchezo unaopendwa na vijana wengi. Alizoea kunyoa nywele zote katika kichwa chake na kuachwa na kipara. Vijana waliompenda walianza kunyoa kama yeye kama kitambulisho chao. Hali hii ilileta upanuzi wa maana kwa kuwa sasa mbali na kumrejelea *Jordan*, neno hili pia lilitumiwa kumaanisha kichwa kilichonyolewa upara.

Neno la pili, limetoholewa kutoka kwa lugha ya Gikuyu. *Muruthi* ni neno linalotumiwa kumrejelea simba, mnyama wa mwituni, mkubwa ambaye ni wa jamii ya paka na mwenye manyoya ya maji makavu. Dhana hii inapotumiwa na wanasheng' ina maana mbili. Maana ya kwanza ni kuashiria mtu mkali ambaye anaogopwa kama vile simba huogopwa na wanyama wengine. Maana ya pili inarejelea gari lililotengenezewa nchini Ufaransa, na ambalo limechorwa alama ya simba kama nembo yake.

Neno *Rambo* limetokana na jina la binadamu la lakabu. Huyu ni mtu aliyetoa kanda nyingi za filamu za vita na anajitambulisha kwa jina hili. Kwa kawaida sinema zake huonyesha vita na mauji ya watu wengi huku *Rambo* akiibuka mshindi kila wakati. Wanasheng' wanatumia neno hili kumrejelea mtu yeyote mkali ambaye anaweza kushinda watu katika vita kama Rambo. Neno hili pia humrejelea mtu mwenye nguvu za kimwili na uwezo wa kutumia viungo vyake vizuri hasa katika vita.

Neno *njogu* lilitokana na lugha ya Gikuyu. *Njogu* ni mnyama anayeitwa ndovu kwa Kiswahili. Huyu ni mnyama mkubwa sana wa porini mwenye mkonga na pembe zenye thamani ya juu. Wanasheng' wanatumia jina hili kurejelea noti ya shilingi elfu moja za Kenya, au mtu mkubwa zaidi. Jambo hili linatokana na sababu kadha. Kwanza ile noti ya shilingi elfu moja imechorwa alama ya ndovu. Noti hii huwa na thamani ya juu kuliko noti zingine zote humu nchini Kenya. Watu walio wakubwa na ambao wanawashinda wengine kwa kimo pia hurejelewa kwa neno hili kwa kulinganishwa na mnyama huyu.

Upanuzi wa maana ya maneno ya Sheng' ulionekana bayana katika sehemu zilizojadiliwa kutegemea muktadha wa maazungumzo. Mifano iliyotolewa hapo juu inathibitisha jinsi Sheng' inavyojiimarisha katika uwanya wa kisemantiki. Upanuzi wa maana unahakikisha kuwa dhana zilizopo katika lugha zimetumiwa kwa ukamilifu na upana zaidi na kuepusha haja ya kubuni msamiati mpya kila mara. Mbinu nyingine inayotumika zaidi ni ya ufinyizi maana.

**3.0 Ufinyizi maana**

Ufinyizi maana ni dhana inayotumika zaidi katika usemaji wa kila siku. Dhana hii hutumiwa wakati ambapo maana za jumla za maneno hupotea na kurejelea zile maana zilizo bayana zaidi kuliko zamani (Antila 1972) mfano:

**(1.6)**

| **Data** | **lugha changizi** | **tafsiri** |
|---|---|---|
| *Jiji* | Kiswahili | Nairobi |
| *Majuu* | Kiswahili | Marekani |

Neno *jiji* limetokana na lugha ya Kiswahili na linamaanisha mji mkubwa ambao labda ni makao makuu ya serikali. Sehemu hii pia huwa na wakazi wengi pamoja na nyumba nyingi zilizojengwa mahali pamoja. Mifano ya jiji ni kama vile Dar es Salaam, Kampala, Maputo, Cairo na kadhalika. Neno hili hata hivyo linapotumiwa na wanasheng' hurejelea *jiji* la Nairobi pekee. Huu ni mji mkuu wa Kenya ambao ndio makao makuu ya serikali na mashirika mengine ya kimataifa. Ufinyizi maana umetokea katika matumizi ya neno hili kwani kuna miji mingine mikubwa nchini na hata nje ya nchi lakini haipewi jina hili.

Neno majuu linatokana na neno la Kiswahili juu, linalomanisha zaidi ya kingine au kinyume cha chini. Linatoholewa kimofolojia na kuwa majuu kwa kuongezewa kiambishi {ma}. Maana yake katika Sheng' hurejelea nchi ya Marekani. Nchi hii ina uwezo mkubwa kuliko nchi zingine ulimwenguni. Dhana hii ingawa inaweza kurejelea maana zingine, katika mkabala wa wanasheng' linatumika kurejelea taifa la

Marekani pekee na wala sio sehemu zozote zingine za juu. Ufinyizi maana unaweza kuchanganuliwa zaidi kwa kuangazia kategoria zifuatazo:

1. Mahali
2. Pesa
    a. nomino za jumla
    b. nomino za rangi
3. Nomino za kidhahania

### 3.1 Mahali

Mahali ni neno lenye matumizi mbalimbali kwa maana ya sehemu ya ulimwengu. Wanasheng' wametohoa baadhi ya sehemu za nchi kuashiria maana maalum katika usemaji wao. Utohozi huu unaonekana kuchochewa na sababu kadhaa kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

**(1.7)**

| **Data** | **chanzo cha neno** | **maana** |
|---|---|---|
| *Hangare* | nchi ya Hungare | nguo kuukuu |
| *Tokyo* | mji mmoja nchini Japani | Mtu mfupi |
| *Sahara* | Jangwa kubwa barani afrika | Viatu |

*Hangare* ni neno linalotumiwa kurejelea nguo kuukuu zilizonunuliwa kutoka nje. Nguo hizi kwa kawaida huitwa *mitumba* na watu wengi. Nguo nyingi za aina hii zilitoka nchi ya *Hungary*, taifa moja katika bara la Yuropa. Wanasheng' wanatumia jina hili kurejelea aina hii ya nguo. Maana inayolenga nchi inapotea na kubadilishwa kurejelea maana ya nguo kuukuu.

Neno *tokyo* lililotoholewa kutoka jina la mji mkuu wa nchi ya Ujapani. Hili ni taifa lililoko barani Esia. Wenyeji wengi wa nchi hii, huwa na kimo kifupi wakilinganishwa na mataifa mengine. Wanasheng' wametumia dhana hii ya mji kuwakilisha watu walio wafupi. Hapa sifa za mji mkuu wa taifa, zinafinywa na kurejelea watu wafupi pekee. Mfano wa *sahara* umetokana na neno linalotumiwa kurejelea jangwa lililoko barani Afrika linaloitwa Sahara. Hili ni jangwa kubwa lililoko kaskazini mwa bara la Afrika na ambalo limetanda katika mataifa mengi. Jangwa hili lina vumbi nyingi, hali mbaya ya hewa na ukosefu wa mvua na mimea. Wanasheng' wanatumia dhana hii kurejelea aina ya viatu maalum vya wanaume vilivyo na rangi ya manjano au majani makavu. Rangi hii ni kama rangi ya mchanga wa jangwa la sahara. Ngozi yake ni ngumu na huweza kutumiwa kwa muda mrefu bila kuharibika. Hapa inaonekana kuwa jina la jangwa kubwa limefinywa kurejelea aina hii maalum ya viatu.

Kategoria ya pili ni ya nomino za pesa. Pesa huthaminiwa na vijana kwa sababu zinawawezesha kutimiza mambo mengi wanayoyahitaji, kauli ambayo inatiliwa nguvu na maneno mengi yanayopewa viwango mbalimbali vya pesa. Mifano ifuatayo inatoa mwangaza zaidi.

### 3.2 Nomino za pesa

Kuna makundi mawili yanayoashiria ufinyizi wa maana katika kategoria hii:

1. Nomino za jumla
2. Nomino za rangi

Kundi la kwanza linajumuisha nomino za jumla za pesa. Viwango mbalimbali vya pesa hupewa nomino za jumla kupitia ufinyizi wa maana. Hili linamaanisha kwamba nomino ya noti fulani inaweza kutumiwa kutoa maana zingine. Wanasheng' hata hivyo wamefinya maana hizo zingine na kutumia neno lile kuashiria kiwango maalum cha pesa pekee. Hoja hii inaweza kueleweka zaidi katika mifano iliyoko hapa chini:

**(1.8)**

| **Data** | **lugha changizi** | **maana** |
|---|---|---|
| *Ashara* | Kiswahili | shilingi kumi |
| *Iratathi* | Gikuyu | shilingi mia |
| *Finje* | Kiingereza | shilingi hamsini |

*Ashara* ni neno lililotoholewa kutoka kwa lugha ya Kiswahili ambalo linamaanisha kumi. Wanasheng' hata hivyo wanalitumia kumaanisha shillingi kumi pekee na wala sio vitu vingine. Ufinyizi wa maana umetokea hapa kwa sababu kungekuwa na vitu vingine vingi ambavyo vingerejelewa kupitia neno hili. *Iratathi* ni neno la Gikuyu linalomaanisha karatasi yoyote. Karatasi hii inaweza kuwa ya gazeti, barua, kitabu au hata ya kuweka vitu kama ile ya plastiki. Dhana hii imebanwa katika Sheng' kurejelea noti ya shilingi mia moja pekee

Neno finje limetoholewa kutokana na lugha ya Kiingereza. Neno kamili katika lugha hii ni *Fifty*, yaani hamsini. Kupitia mifanyiko ya kifonolojia sauti /t/ na /y/ hubadilishwa na kuwa /ɲє/ ili kuunda neno *finje*. Ufinyizi wa maana umetokea hapa kwa sababu wanasheng' hutumia dhana hii kurejelea shilingi hamsini pekee na wala sio vitu vingine vyenye idadi ya kiasi hiki.

Kundi la pili katika kategoria hii ni lile linalogawa pesa kwa ufinyizi wa maana ya rangi. Rangi mbalimbali zimetumiwa kurejelea noti za pesa, mfano:

**(1.9)**

| **Data** | **thamani ya pesa** |
|---|---|
| iningri | shilingi kumi |
| buluu | shilingi ishirini |
| red | shilingi mia moja |

Hapa nomino za rangi mbalimbali zinatumika kuelezea viwango tofauti vya pesa. *iningri* ni tabadili ya silabi ambayo, ikiwekwa katika hali ya kawaida huwa *green* au rangi ya kijani kibichi. Noti ya shilingi kumi huwa na rangi ya kijani kibichi. Neno hili linapotumika hapa, hurejelea shilingi kumi pekee licha ya kuwa vitu vingi huwa na rangi ya kijani kibichi kama vile nguo, majani, miti, na hata aina fulani ya nyoka.

*Buluu* nayo ni rangi ya noti ya shillingi ishirini. Rangi hii imetumika kuwakilisha kiwango cha shilingi ishirini pekee na wala sio vitu vingine kama vile mbingu au vitu vyenye rangi hii. *Red* ni jina la Kiingereza linalorejelea rangi nyekundu kwa Kiswahili. Wanasheng' hulitumia neno hili kurejelea shilingi mia moja, noti ambayo huwa na rangi nyekundu. Mbali na kategoria hii kuna ile inayohusu nomino za kidhahania.

### 3.3 Nomino za kidhahania

Nomino za kidhahania ni zile ambazo haziwezi kuhisika kwa fahamu za kawaida. Uwepo wa nomino hizi unaeleweka tu kupitia nafsia za binadamu. Mgullu (1999) amefafanua kategoria hii kama mojawapo wa nomino za Kiswahili zinazojidhihirishwa kupitia mgao wa kisemantiki. Baadhi ya maneno katika kategoria hii, yanapotumika katika Sheng' yanadhihirisha ufinyizi wa maana, mathalan:

**(1.10)**

| **Data** | **lugha changizi** | **tafsiri ya maana** |
|---|---|---|
| *ukiri* | Gikuyu | ukimwi |
| *hewa* | Kiswahili | muziki |
| *goro* | Gikuyu | dhahabu |

Neno *ukiri* limetokana na lugha ya Gikuyu kumaanisha woga. Mtu anaweza kuwa na hofu ya kukumbwa na jambo la kutisha au taabu. Wanasheng' wamelitumia neno hili kurejelea ugonjwa sugu wa ukimwi. Huu ni ugonjwa wa zinaa usiokuwa na tiba ambao umewaua mamilioni ya watu duniani. Mtu anapougua ugonjwa huu huogopwa sana na wengine na hata hutorokwa na marafiki zake. Wanasheng' hutumia dhana hii kurejelea ugonjwa huu hatari licha ya kuwa neno hili linaweza kutumika kuonyesha hofu zingine.

*Hewa* hutokana na neno la Kiswahili linalorejelea upepo mwororo unaozunguka ardhi. Upepo huu huwa unavutwa na viumbe ili waendelee kuishi. Dhana hii imetoholewa na wanasheng' kumaanisha muziki. Sababu moja ni kuwa vijana hupenda muziki na wanapoukosa ni kama kukosa uhai unaoletwa na muziki huu. Neno hili limetumika kuwakilisha hali hii. Ufinyizi wa maana umetokea hapa kwani hewa inatumika kurejelea muziki pekee katika Sheng'.

Neno lingine ni *goro*. Hili ni neno la Gikuyu linalotumiwa kumaanisha thamani kubwa au enye bei ya juu. Wanasheng' wanalitumia neno hili kurejelea dhahabu. Hii ni aina ya madini iliyo na thamani kubwa duniani na ambayo ina rangi ya manjano. Madini haya hutumika kutengenezea vyombo vya thamani ya juu kama vile sarafu, mapambo na hata medali. Ufinyizi wa maana unatokea katika utohozi wa dhana hii kwa sababu kuna vitu vingi vya dhamani kubwa. Wanasheng' hata hivyo wametumia dhana hii kurejelea madini ya dhahabu pekee.

Sehemu hii imethibitisha wazi kwamba ufinyizi maana hutumika kama mbinu muhimu ya utohozi katika lugha ya Sheng'. Ufinyizi huu unaonekana kutokea kufuatia misingi maalum ya ubunifu kama ilivyodhibitishwa na ufafanuzi huu. Mbinu hii hutumika kwa jumla na lugha ili kuirahisisha. Mantiki hapa ni kuwa mawazo hulenga kudondoa dhana zisizo na umuhimu mkubwa wa kimaana na kubakisha zile zinazolenga ndipo katika kufafanua dhana mbalimbali.

## HITIMISHO

Makala hii imechambua aina tatu za utohozi wa maana katika msimbo wa Sheng' Aina hizi ni pamoja na usogezi maana, Upanuzi maana, na ufinyizi wa maana. Uchunguzi wetu ulidhihirisha kuwa kuna taratibu maalum, na zenye mantiki ambazo zinatumiwa na wanasheng' katika kutohoa maana za leksia mbalimbali wanazotumia. Aidha, ubunifu wao wa hutumika katika kufafanua msamiati mpya unaozuka kila siku kutokana na sababu mbalimbali. Uchunguzi wa kina katika sehemu hii unaweza kudhihirisha falsafa za wanasheng' kuhusu maisha yao pamoja na miondoko yao. Ilidhihirika kuwa utohozi wao wa kisemantiki si wa kiholela bali unafuata mantiki Fulani huku mbinu mahsusi za kisemantiki kama vile metonimu na

sinedochi zikitumika. Hizi ni mbinu zinazoweza kutumika katika lugha nyingine yoyote ile.

**MAREJELEO**


1. Aswani, B.K., Njogu, & Mwihaki, A.N. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
2. Chimerah, R. (1988). *Kiswahili: Past, Present and Future*. Nairobi: Nairobi University Press.
3. Dijk, V.T. (1977). *Text and Context: Explorations in the Semantics and Pragmatics of Discourse*. London: Longman.
4. Echessa. (1990). "A study of the Word Structure and Process Involved in Word Formation in Sheng'. A Case Study of Eastlands area in Nairobi"**.** (Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta Univeristy).
5. Fink, T.K. (2005). "Attitudes towards Languages in Nairobi". <http://etd.library.pitt.edu/ETD/available/etd-04212005-12.428/> Tarehe ya upakuaji 7/7/2007
6. Gachinu, J.N. (1996)." Linguistic Aspects of Code-switching in Gikuyu". (Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University).
7. Githinji, P. (2006). "Bazes and Their Shibboleths: Lexical Variation and Sheng' Speakers' Identity in Nairobi".<http://www.njas.Helsinki.fi/pdf-files/vol15num4/githinji.pdf> Tarehe ya upakuaji 10/6/2007
8. Habwe, J. & Peter, K. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
9. Jackson, H., & wengine. (2000). *Words, meaning and vocabulary English*. Trowbridge: Cromwell Press.
10. Kamau, W. (1996). "Relationship between Sheng' and the nature of Kiswahili in Schools". (Unpublished P.G.D.E. Thesis of Kenyatta University).
11. Leech, G.N. (1981). *Semantics*. Hand Worth: Penguin.
12. Lehmann, W.P. (1962). *Historical Linguistic*. New York. Holt, Rinehart and Winston Inc.
13. Locke, T. (2004). *Critical Discourse Analysis*. London: Cromwell Press.
14. Massamba., & Wengine. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
15. Mbaabu, I., & Nzunga, M.P.K. (2003_. *Sheng': Its major Characteristics and Impact in Standard Kiswahili and English***.** Dar es Salaam. TUKI.
16. Mgullu, S.R. (1999) Mtalaa *wa Isimu*. Nairobi: Longhorn.
17. Mokaya, B. (2005). "Hybrid languages: The case of Sheng'" <http://www.lingref.com/cpp/acal/36/paper1423.pdf >Tarehe ya upakuaji 13/4/2007
18. Munuku, A.W. (2005). "Code Switching in the Contemporary Kiswahili Rap Song". (Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University).
19. Mwihaki, A.N. (1998). "Loanword Nativisation: A generative view of the Gikuyu Loanwords." Tasnifu ya uzamifu ya chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
20. Mwihaki, A.N. (2004). "A Functional View of Linguistic Meaning with Reference to Kiswahili", in Kiswahili Vol. 66 No. 2. Dar es Salaam: TUKI.
21. Mwihaki, A.N. (2006). "Sheng" na Usomi wa Kiswahili, Mtazamo wa Kiisimu Jamii". (Makala ya semina ya isimu jamii ambayo ilitolewa Mjini Nakuru. Haijachapishwa).
22. Nyauncho, O. (1986). "An Investigation into the Social and Structural Aspects of an Evolving Language". (Unpublished M.A. Thesis: University of Nairobi).
23. Ogechi, N. (2005). "Lexicalisation in Sheng"<http://www.(nja.helsinki.fi//pdf-files/vol.14nom3/ogechi.pdf> tarehe ya upakuaji 25/3/07.
24. TUKI. (1996). *English-Swahili Dictionary*. Dar-es-Salaam: TUKI.